

Ilani kuhusu Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka

ILANI IMETOLEWA HAPA kwa Wenyehisa kwamba, kwa mujibu wa kanuni za sehemu ya 280 ya Sheria ya Kampuni ya 2015 na kwa mujibu wa Agizo la Mahakama lililotolewa na Mahakama ya Kuu ya Kenya katika Ombi la Ziada Nambari. E680 la 2020 siku ya Jumatano, tarehe 29 Aprili, Mkutano Mkuu wa Sitini na Saba wa Kampuni ya Kenya Electricity Generating Company Plc utafanywa kupitia mawasiliano ya kielektroniki siku ya Jumanne tarehe 3 Novemba 2020, saa tano asubuhi. kwa madhumuni ya kuzingatia na, ikiwa itakuwa vyema, kupitisha maamuzi yaliyobainishwa hapa chini:

SHUGHULI YA KAWAIDA

1. Kuweka bayana majina ya washirika na kutambua uwepo wa idadi ya kutosha ya wanachama ili kuendesha mkutano.
2. Kusoma Taarifa inayoitisha mkutano.
3. Kuzingatia na ikiidhinishwa, kutekeleza Taarifa za Kifedha za Kampuni zilizofanyiwa ukaguzi kwa mwaka uliokamilika tarehe 30 Juni 2019, pamoja na Ripoti za Mwenyekiti, Wakurugenzi Wakuu na Wakaguzi zilizoko.
4. Kuidhinisha malipo ya mgao wa mwisho wa mapato ya hisa ya 10% au Kshs.0.25 kwa kila hisa ya kawaida ya Kshs.2.50, kutegemea ushuru unaoshikiliwa panapotumika, kuhusiana na mwaka wa kifedha uliokamilika tarehe 30 Juni 2019.
5. Kuidhinisha malipo ya ada za Wakurugenzi Wakuu kwa mwaka uliokamilika tarehe 30 Juni 2019.
6. **Wakaguzi wa Kifedha:**

Kubaini kuwa ukaguzi wa vitabu vya akaunti za Kampuni utaendelea kufanywa na Mkaguzi Mkuu au na shirika la ukaguzi atakaloliteua kwa mujibu wa Sehemu ya 23 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya 2015.
7. Kuidhinisha Wakaguzi Wakuu kusuluhisha malipo kwa Wakaguzi wa Kifedha.
8. Kwa mujibu wa kanuni za Sehemu ya 769 ya Sheria ya Kampuni ya 2015, wakurugenzi wakuu wafuatao kwa kuwa wanachama wa kamati ya Bodi ya Ukaguzi, Hatari na Utifu wanachaguliwa kuendelea kuhudumu kama wanachama wa kamati zilizotajwa:

- (i) Bw. Joseph Sitati
- (ii) Bw. Humphrey Muhu, Mwakilishi wa Ukur Yatani (Waziri – Wizara ya Fedha)
- (iii) Bi. Phyllis Wakiaga (Kutegemea iwapo atachaguliwa tena katika Bodi kulingana na Ajenda ya kipengee cha 9 (iii))
- (iv) Bw. Kairu Bachia

9. Kuchagua Wakurugenzi Wakuu:

- (i) Dkt. Mhandisi. Joseph Njoroge, Katibu wa Kudumu, Idara ya Kawi, ambaye anastaafu kwa mzunguko kwa mujibu wa Kifungu cha 104 cha Makala ya Ushirika ya Kampuni na kwa kuwa anastahili, anajitolea kuchaguliwa tena kama Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni.
- (ii) Bi. Phyllis Wakiaga, ambaye anastaafu kwa mzunguko kwa mujibu wa Kifungu cha 104 cha Makala ya Ushirika ya Kampuni na kwa kuwa anastahili, anajitolea kuchaguliwa tena kama Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni.
- (iii) Bw. Joshua Choge ambaye anastaafu kwa mzunguko kwa mujibu wa Kifungu cha 104 cha Makala ya Ushirika wa Kampuni na hajajitolea kuchaguliwa tena kama Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni.
- (iv) Bi. Ziporah Ndegwa, ambaye anastaafu kwa mzunguko kwa mujibu wa kifungu cha 104 cha Makala ya Ushirika ya Kampuni na hajajitolea kuchaguliwa tena kama Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni.

10. SHUGHULI MAALUM:

Kuzingatia na, ikiidhinishwa, kupitisha Uamuzi Maalum:

- (i) “Kwamba Kanuni ya Ushirika wa Kampuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka Kifungu kifuatacho baada tu ya Kifungu cha sasa cha 54 na kuita Kifungu hicho Kipya kuwa Kifungu cha 54A kama ifuatavyo:

Kifungu cha 54A

Wanachama wanaweza, ikiwa watafikiri ni sawa, kuendesha au kufanya mkutano kupitia redio, simu, televisheni, mkutano wa video au kifaa chochote cha

Ilani kuhusu Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka

kielektroniki, au njia nyingine za mawasiliano ya sauti/picha, au mchanganyiko wazo ("Mkutano"). Licha ya kwamba Wanachama hawako pamoja wakati wa Mkutano, uamuzi utakaopitishwa na Wanachama ambao wamefikisha idadi inayohitajika katika Mkutano kama huo basi utachukuliwa kuwa umepitishwa katika Mkutano Mkuu uliofanyika siku na wakati ambapo Mkutano ulifanywa. Kanuni hizi zinazohusiana na Kifungu na vikao vya Wanachama zinatumiwa kadri zinavyoweza kutekeleza hitaji la kubadilisha masuala yanayohitajika kubadilika katika Mkutano kama huo.

- (ii) "Kwamba Kanuni ya Ushirika wa Kampuni ifanyiwe marekebisho kwa kuingiza Kifungu kifuatacha mara tu baada ya Kifungu cha sasa cha 108 na kuita Kifungu kipya kama Kifungu cha 108A kama ifuatavyo:

Kifungu cha 108A

Wakurugenzi Wakuu wanaweza, ikiwa watafikiri kuwa ni sawa, kuendesha au kufanya mkutano kupitia redio, simu, televisheni, mkutano wa video au njia nyingine za kielektroniki, njia za mawasiliano za sauti/picha, au mchanganyiko wazo ("Mkutano"). Licha ya kwamba Wakurugenzi hawapo pamoja wakati ambapo Mkutano unaendeshwa, uamuzi utakaopitishwa na Wakurugenzi waliotimiza idadi hitajika katika Mkutano kama huo utachukuliwa kuwa umepitishwa katika mkutano wa Bodi utakaofanywa siku na wakati ambapo Mkutano huu utafanywa. Kanuni hizi zinazohusiana na Kifungu na vikao vya Wakurugenzi zinatumiwa kadri zinavyoweza kutekeleza hitaji la kubadilisha masuala yanayohitajika kubadilika katika Mkutano kama huo.

11. Kuzingatia shughuli nyingine yoyote ambayo taarifa yake imetolewa.

Kwa Agizo la Bodi



Paul K. Ndungi
Katibu wa Kampuni

Tarehe 8 Oktoba 2020

VIDOKEZO:

Wenyehisa wataweza kujisajili ili kufuatilia mkutano,

kupiga kura kwa njia ya kielektroniki au kupitia washirika na wanaweza kuuliza maswali mapema kabla ya tarehe ya Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka kwa namna iliyobainishwa ifuatavyo:

- (i) Kutokana na janga tandavu linaloendelea la Virusi vya korona 2019 (COVID-19) na Kanuni Zinazohusiana na Afya ya Umma na maagizo yaliyopitishwa Serikali ya Kenya kuzuia mikutano ya hadhara, si rahisi, kwa KenGen kufanya Mkutano Wake Mkuu wa Kila Mwaka wa ana kwa ana kwa njia iliyobainishwa katika Kanuni ya Ushirika wa Kampuni na sehemu ya 280 ya Sheria ya Kampuni ya 2015. Mnamo tarehe 29 Aprili 2020, Mahakama Kuu ya Kenya katika Ombi la Ziada Nambari. E680 ya 2020, lililotolewa linaloruhusu kampuni yoyote iliyoorodheshwa katika Soko la Hisa la Nairobi kufanya mkutano na kuendesha mkutano mkuu mtandaoni baada ya kupokea 'Hakuna Pingamizi' kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mtaji ('CMA'). Kwa kutegemea agizo hili la mahakama, KenGen imefanya na itaendesha mkutano wake mkuu wa kila mwaka mtandaoni baada ya kupokea 'Hakuna Pingamizi' kutoka CMA.
- (ii) Wenyehisa ambao wangependa kushirika katika mkutano huu wanapaswa kujisajili kwa ajili ya mkutano wa mkutano mkuu wa kila mwaka kwa kupiga *483*820# kwenye simu zao za mkononi na kufuata maagizo mbalimbali yanayoibuka katika mchakato wa usajili.
- (iii) Ili kukamilisha mchakato wa kujisajili, wenye hisa watahitaji kutoa Nambari za Kitambulisho cha Kitaifa/Pasipoti ambayo walitumia kununua hisa zao na/ au Nambari Yao ya Akaunti ya CDSC. Kwa usaidizi, Wenyehisa wanapaswa kupiga nambari ifuatayo ya usaidizi: +254 709170 000/709170 016 kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa tisa jioni kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Wenyehisa walio nje ya Kenya wanapaswa kupiga nambari ya usaidizi ili kupata usaidizi wakati wa usajili.
- (iv) Usajili kwa ajili ya mkutano mkuu wa kila mwaka unafunguliwa siku ya Ijumaa, tarehe 9 Oktoba 2020 saa tatu asubuhi na utafungwa Jumamosi, tarehe 31 Oktoba 2020 saa kumi na moja jioni. Wenyehisa hawataweza kujisajili baada ya wakati huu.
- (v) Kwa mujibu wa Kifungu cha 137 cha Kanuni ya Ushirika wa Kampuni, hati zifuatazo zinaweza kutazamwa kwenye wavuti ya Kampuni www.kengen.co.ke
(a) nakala ya Taarifa hii na Fomu ya Mshirika;
(b) Ripoti ya Kila Mwaka na Taarifa za Kifedha

Ilani kuhusu mkutano mkuu wa Kila mwaka

- Zilizokaguliwa za Kampuni za mwaka uliokamilika tarehe 30 Juni 2019;
- (c) nakala ya Agizo la Mahakama Kuu katika Ombi la Ziada Nambari E680 la 2020; na
- (d) nakala ya 'Hakuna Pingamizi' iliyotolewa na CMA.
- (vi) Mwenye hisa yeyote ambaye ana haki ya kuhudhuria na kupiga kura katika Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka ana haki ya kuteua mshirika kuhudhuria na kupiga kuwa kwa niaba yake. Si lazima mshirika kama huyo awe mwachama wa Kampuni.
- (vii) Fomu ya Mshirika imetolewa pamoja na Ripoti ya Kila mwaka na Akaunti. Fomu ya Mshirika pia inaweza kupatikana kutoka kwenye tovuti ya Kampuni www.kengen.co.ke au kutoka Image Registrars Limited, Jumba la Absa (lililokuwa Jumba la Barclays), Orofa ya 5, Barabara ya Loita, S.L.P 9287 – 00100, Nairobi, Kenya. Wenye hisa ambao hawangependa kuhudhuria Mkutano mkuu wa Kila Mwaka wana chaguo la kukamilisha na kurejesha Fomu ya Mshirika kwa Image Registrars Limited, au vinginevyo kwa Ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni ili ifike sio baada ya saa tano asubuhi tarehe 1 Novemba 2020.
- (viii) Fomu za mshirika zilizotiwa sahihi ifaavyo pia inaweza kutumwa kwa KenGen Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka@ image.co.ke katika umbizo la PDF. Fomu ya mshirika lazima itiwie sahihi na mteuzi au wakili wake ambaye amehalalishwa kupitia maandishi. Ikiwa mteuzi ni shirika, chombo kinachoteua mshirika kitatolewa chini ya muhuri ya kawaida ya Kampuni au chini ya mkono wa afisa au wakili aliyehalalishwa wa shirika kama hilo.
- (ix) Wenye hisa ambao wangependa kuuliza maswali yoyote au ufafanuzi kuhusiana na mkutano mkuu wa kila mwaka wanaweza kufanya hivyo mnamo au kabla ya tarehe 1 Novemba 2020 saa tano asubuhi:
- (a) kutuma maswali yaliyoandikwa kupitia barua pepe kwa agmquestions@kengen.co.ke; au
- (b) kadri iwezekanavyo, kuleta maswali yao yaliyoandikwa wao wenyewe mahali halisi, anwani ya posta au ya barua pepe kwenye ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni au S.L.P 47936 – 00100, Nairobi, au katika ofisi za Image Registrars kwa S. L.P 9287 – 00100, Nairobi, Kenya.
- Ni lazima wenye hisa watoe maelezo yao kamili (majina kamili, Kitambulisho cha Kitaifa/Nambari ya Pasipoti/ Nambari ya Akaunti ya CDSC) wanapowasilisha maswali au ufafanuzi wao.
- Wakurugenzi wa Kampuni watatoa majibu yaliyoandikwa ya maswali yaliyopokewa kwenye anwani ya mahali halisi, anwani ya posta au ya barua pepe iliyotolewa na Wenye hisa sio baada ya saa 12 kabla ya kuanza kwa mkutano mkuu wa kila mwaka. Orodha kamili ya maswali yaliyopokewa na majibu yaliyofuata baadaye yatachapishwa kwenye wavuti wa Kampuni sio baada ya saa 12 kabla ya kuanza kwa Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka.
- (x) Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka utaonyeshwa mubashara au moja kwa moja kupitia kiungo ambacho kitatolewa kwa wenyehisa wote ambao wamejisajili kushiriki katika Mkutano huo Mkuu wa Kila Mwaka. Wenyehisa waliosajiliwa halali na washirika watapokea ujumbe mfupi (SMS)/USSD kwenye nambari zao za simu zilizosajiliwa, saa 24 kabla ya mkutano mkuu wa kila mwaka kuanza hii ikiwa ni kikumbusho kuhusu mkutano mkuu wa kila mwaka. Ujumbe wa pili wa SMS/USSD utatumwa saa moja kabla ya mkutano mkuu wa kila mwaka, ukiwakumbusha wenye hisa na washirika waliosajiliwa halali kwamba mkutano mkuu wa kila mwaka utaanza baada ya saa moja na kutoa kiungo cha kutiririsha moja kwa moja.
- (xi) Wenye hisa na washirika wao ambao wamejisajili kushiriki katika mkutano mkuu wa kila mwaka wanaweza kufuatilia vikao kwa kutumia jukwaa la kutiririsha moja kwa moja, kufikia agenda na kupiga kura Mwenyekiti akiwaomba kufanya hivyo kupitia USSD.
- (xii) Matokeo ya maamuzi yaliyopigiwa kura yatachapishwa kwenye wavuti wa Kampuni ambao ni, www.kengen.co.ke ndani ya saa 24 baada ya kuhitimishwa kwa mkutano mkuu wa kila mwaka.
- Wenye hisa wanahimizwa kuendelea kufuatilia wavuti wa Kampuni kwa taarifa zozote zinazohusiana na mkutano mkuu wa kila mwaka kwa sababu ya hali inayobadilika kutokana na janga la COVID-19. Tunathamini uelewa wa washikadau wetu huku tukipitia hali zinazobadilika za biashara zilizosababishwa na COVID-19.